Guilford COUNTY SCHOOLS

Kutoka: Guilford County Schools (GCS)
Tarehe: Tarehe 1 Agosti 2025
Kuh: Barua na Taarifa ya Haki ya Kujua ya Wazazi

Kama mzazi wa mwanafunzi aliye katika shule ya Mpango wa Title I katika Guilford County Schools (GCS) na kama sehemu ya taarifa yetu ya mwanzo wa kila mwaka wa shule, una haki ya kujua kuhusu (1) sifa za kitaaluma na vigezo vya kuwa na leseni vya walimu wanaomfundisha mtoto wako, (2) taarifa kuhusu ushiriki wa mwanafunzi katika mitihani ya lazima ya Jimbo au ya eneo na sera zinazohusiana, (3) mafundisho ya lugha na taratibu na huduma za kutambua wanafunzi wa Kiingereza, na hakikisho letu, kwamba taarifa hiyo itatolewa katika lugha inayoeleweka na muundo unaoweza kufikiwa. Hili ni sharti kwa shule zote za umma (Public School Units, PSU) zinazopokea fedha kutoka kwa Mpango wa Title I na hukuruhusu kuomba taarifa hiyo na kupokea jibu kwa wakati ufaao. Hapa chini kuna maelezo zaidi kuhusu taarifa ya Haki ya Kujua ya Wazazi.

(1) Sifa za Kitaaluma na Vigezo vya Kuwa na Leseni vya Walimu
   a. Guilford County Schools (GCS) inawafahamisha wazazi kwamba wana haki ya kuomba taarifa kuhusu sifa za kitaaluma za walimu wa darasa la mwanafunzi wao, na jibu letu litatolewa kwa wakati ufaao, ikijumuisha taarifa ifuatayo na kama mwalimu wa mwanafunzi—
      i. ametimiza sifa zinazohitajika na vigezo vya kuwa na leseni vya Jimbo kwa viwango vya madarasa na mada za masomo ambazo mwalimu huyo hufundisha,
      ii. anafundisha chini ya hali ya dharura au hali nyingine ya muda ambapo sifa zinazohitajika au vigezo vya kuwa na leseni vya Jimbo vimeondolewa, na
      iii. anafundisha katika sehemu ya kitaaluma inayolingana na utaalamu wa mwalimu huyo.
   b. Ikiwa mtoto anapewa huduma na wasaidizi wa wataalamu na, ikiwa ni hivyo, sifa zao.
   c. Taarifa kuhusu kiwango cha mafanikio na ukuaji wa kielimu wa mwanafunzi, ikiwa unahusika na unapatikana, kwenye kila tathmini ya kielimu ya Jimbo inayohitajika; na
   d. Kupewa taarifa kwa wakati unaofaa kwamba mtoto wako amefundishwa kwa wiki 4 au zaidi mfululizo na mwalimu ambaye hatimizi sifa za kitaaluma zinazohitajika ili kuidhinishwa au masharti ya kuwa na leseni ya Jimbo katika kiwango cha darasa na somo alilokabidhiwa.

(2) Uwazi na Taarifa Kuhusu Mitihani, Ushiriki wa Wanafunzi katika Mitihani ya Lazima ya Jimbo au Eneo, na Sera Zinazohusiana
   a. Wazazi wanaweza kuomba na kupokea jibu kwa wakati ufaao, taarifa kuhusu sera yoyote ya Jimbo au shule ya eneo kuhusu ushiriki wa mwanafunzi katika tathmini zozote za lazima na taratibu zinazohusiana, au haki ya mzazi ya kukataa mtoto wake asifanye tathmini hiyo, inapohitajika.
   b. Guilford County Schools (GCS) itahakikisha taarifa inapatikana kwa umma waziwazi kupitia njia na taarifa za umma, ikijumuisha kwa kuchapisha kwa njia wazi na inayoweza kufikiwa kwenye tovuti yetu kuhusu kila darasa linalohudumiwa na kutoa taarifa kuhusu kila tathmini kama inavyotakiwa na Jimbo na eneo, ili kutii kanuni pale ambapo taarifa hizo zinapatikana na inawezekana kuziripoti, ikiwa ni pamoja na—
      i. somo lililotathminiwa,
      ii. kusudi la kuunda na kutumia tathmini,
      iii. chanzo cha masharti ya tathmini, na
      iv. pale ambapo taarifa hizo zinapatikana—
         1. muda ambao wanafunzi watatumia kufanya tathmini na ratiba ya tathmini; na

2. muda na muundo wa kusambaza matokeo.

(3) Mafundisho ya Lugha na Taratibu na Huduma za Kutambua Mwanafunzi wa Kiingereza

a. Ndani ya kipindi kisichozidi siku 30 baada ya kuanza kwa mwaka wa shule Guilford County Schools (GCS) itawajulisha wazazi kuhusu mwanafunzi wa Kiingereza aliyetambuliwa kushiriki katika mpango huo na kuwaambia taarifa ifuatayo—
   i. sababu za kutambuliwa kwa mtoto wao kama mwanafunzi wa Kiingereza na anayehitaji kuwekwa katika mpango wa elimu wa mafundisho ya lugha,
   ii. kiwango cha mtoto cha ustadi wa Kiingereza, jinsi kiwango hicho kilivyotathminiwa, na hali ya mafanikio ya kielimu ya mtoto,
   iii. mbinu za kufundisha zinazotumiwa katika mpango ambapo mtoto wao anashiriki au atashiriki na mbinu za kufundisha zinazotumiwa katika mipango mingine inayopatikana, ikiwemo jinsi mipango hiyo inavyotofautiana katika maudhui, malengo ya mafunzo, na matumizi ya Kiingereza na lugha ya asili katika mafundisho,
   iv. jinsi ambavyo mpango ambapo mtoto wao anashiriki, au atashiriki, utashughulikia uwezo wa kielimu na mahitaji ya mtoto wao,
   v. jinsi ambavyo mpango huo utamsaidia hasa mtoto wao kujifunza Kiingereza na kufikia viwango vya kufaulu kielimu vinavyohitajika ili kuruhusiwa kwenda katika darasa linalofuata na kuhitimu,
   vi. masharti maalum ya kuondoka kwenye mpango, ikiwa ni pamoja na kiwango kinachotarajiwa cha kuondoka kwenye mpango huo na kurudi kwenye madarasa ya kawaida ambayo hayajaundwa kwa ajili ya wanafunzi wa Kiingereza na kiwango kinachotarajiwa cha kuhitimu kutoka shule ya upili,
   vii. katika hali ya mtoto mwenye ulemavu, jinsi mpango na huduma hizo zinavyofikia malengo ya mpango wa elimu wa mtu binafsi wa mtoto huyo, na
   viii. taarifa kuhusu haki za wazazi ambayo inajumuisha mwongozo ulioandikwa:
      1. unaoeleza haki ya wazazi ya kumwondoa mtoto wao kwenye mpango huo mara moja baada ya ombi lao,
      2. unaoeleza machaguo ya wazazi ya kukataa kuandikisha mtoto wao katika mpango huo au kuchagua mpango au mbinu nyingine ya mafundisho, ikiwa inapatikana, na,
      3. kuwasaidia wazazi kuchagua mipango na mbinu mbalimbali za mafundisho ikiwa zaidi ya mpango/mbinu 1 inatolewa.

b. Kanuni Maalum Wakati wa Mwaka wa Shule—Kwa watoto waliotambuliwa kuwa wanafunzi wa Kiingereza katika mwaka wa sasa wa shule Guilford County Schools (GCS) itawaarifu wazazi wa watoto hao ndani ya wiki 2 za kwanza baada ya mtoto kuwekwa katika mpango wa elimu wa mafundisho ya lugha.

c. Ushiriki wa Wazazi Guilford County Schools (GCS) itatekeleza njia mwafaka za kuwafikia wazazi wa wanafunzi wa Kiingereza ili kuwajulisha wazazi hao—
   i. jinsi wanavyoweza kushiriki katika elimu ya watoto wao; na
   ii. kuwa washiriki wanaohusika kikamilifu katika kuwasaidia watoto wao—
      1. kupata ustadi wa Kiingereza,
      2. kufikia viwango vya juu katika elimu kamilifu; na kufikia viwango vya elimu vya Jimbo vinavyotia changamoto vinavyotarajiwa kwa wanafunzi wote.
   iii. Guilford County Schools (GCS) imejitolea kutekeleza njia mwafaka za kuwafikia wazazi, ambazo ni pamoja na kufanya mikutano na kutuma taarifa kuhusu fursa za mikutano ya mara kwa mara ili kuunda na kushughulikia mapendekezo kutoka kwa wazazi wa Wanafunzi wa Kiingereza.

Kiambatisho cha C

Tafadhali wasiliana na **ofisi ya Mpango wa Title I kwa 336-370-2368** kwa maombi au maswali au maelezo zaidi. Asante.

Guilford COUNTY SCHOOLS

Tarehe:

KWA: Wazazi/Wanafamilia/Walezi

KUTOKA:

KUH: SIFA ZA KITAALUMA NA LESENI ZA WALIMU

Kwa mujibu wa Sheria ya Kila Mwanafunzi Anapaswa Kufaulu (Every Student Succeeds Act, ESSA) na kando na taarifa yetu ya kina ya Haki ya Kujua ya Wazazi ya mwanzo wa mwaka, kila mzazi na mwanafamilia atapewa taarifa kwa wakati ikiwa mtoto wao amepewa au amefundishwa kwa wiki nne au zaidi mfululizo na mwalimu ambaye hatimizi sifa zinazohitajika au masharti ya kuwa na leseni ya jimbo yanayotumika kulingana na kiwango alichopewa cha darasa/somo/mada ya maudhui.

Taarifa hii ni ya kukujulisha kuwa mwalimu(walimu) aliye hapa chini amepewa jukumu la kuwa mwalimu wa mtoto wako au amemfundisha mtoto wako kwa wiki nne au zaidi mfululizo huku akiwa hatimizi sifa zinazohusika au masharti ya kuwa na leseni katika kiwango cha darasa/somo/mada ya maudhui kulingana na kazi aliyopewa:

| Jina la Mwalimu | Hatimizi Masharti ya ESSA (x) | Kiwango(Viwango) cha Darasa Alilopewa | Somo/Mada ya Maudhui |
|---|---|---|---|
| Justin Example | x | Darasa la 4 | Hisabati, Sanaa ya Lugha ya Kiingereza |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

(Add content as applicable) Ingawa mwalimu wa mtoto wako kwa sasa hana leseni ya kufundisha na sifa zinazohitajika, tunatoa hakikisho/tunaamini...

(Add content as applicable) Zaidi ya hayo, kuna mpango unaotumika ili... (k.v., kuwezesha utendakazi wa mwalimu, kuhakikisha kwamba mtoto wako anapokea mafundisho bora, nk.).

Ikiwa una maswali yoyote yanayohusiana, tafadhali wasiliana nami haraka uwezavyo kupitia nambari XXX-XXX-XXXX.

Kwa Dhati,

Name
Title
Signature